

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

IBILISI, KAMA SIMBA ANGURUMAYE

Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani . . .—1 Petro 5:8.

Hapo mwaka wa 1898 barabara ya reli ilikuwa ikijengwa kupitia Bonde Kuu la Ufa ambalo limeenea toka Kenya hadi Uganda. Kazini humo kulikuwa na maelfu ya watu ambao walishikirishwa katika ujenzi wa reli hiyo na pia kulikuwa na mahali kwingi ambako kambi zilisimamishwa ambazo ndizo zilikuwa malazi ya wafanyi kazi hao. Lakini wafanya kazi hao wakaanza kutoweka mmoja baada ya mwingine, na punde si punde ikatambuliwa kwamba kulikuwa na simba wawili wala watu wa kutoka bunga la Tsavo. Simba hao waliendelea kuleta rabsha kwa muda wa miezi tisa, na wakawauwa watu wengi na kufanya maelfu ya wafanyi kazi kuishi katika hali ya woga. Wafanyi kazi hao wakajaribu kujenga mipaka ya miiba kuzungukia kambi zao na pia kuwasha mioto usiku ili kufanya simba hao kuwa na woga, lakini simba wenyewe waliweza kuruka na kuvuka mipaka hiyo, ama wakapita kwenye mianya ya mipaka ya miiba. Basi simba wangewavamia watu kwenye hema hizo na kuwavuta kuwapeleka vichakani ambako mara nyingi walisikika wakiwavunja-vunja waadhiriwa hao mifupa huku wakitoa migurumo ya kushiba. Hebu fikiria woga ambao hata kama ni wewe ungekupata kama ungetembea gizani huku ukijua kwamba simba mla watu alikuwa amejificha kwenye kichaka kilichokuwa karibu nawe.

Wakati mwingi simba hao wangesikika wakinguruma hapo karibu na moja ya kambi hizo na habari hiyo ingesambaa kutoka kambi moja hadi nyingine: “Tahadhari ndugu, shetani anakuja!” Mara moja mlio mkubwa

wa maumivu ungesikika na mtu mmoja zaidi angepunguka kati ya wafanya kazi ambao wangepika kazini asubuhi iliyofuata. Mwisho kabisa ni hapo baada ya watu wengi kuuawa ndipo simba hao waliweza kuuawa.

Mtume Petro anatukanya kwamba tunahitaji kuwa watu wenye kiasi na tuwe makini huku tukijua kwamba shetani ni simba anayenguruma. Shetani, kama simba hao wawili wa Tsavo anajaribu kufanya Wakristo kuishi kwa woga na kufanya juu chini kuua, kuiba, na hata kuangamiza maisha yetu ya kiroho. Basi ni jambo muhimu kwamba tuwe macho na kujichunguza kwa makini ili tutambue wakati ambapo Shetani anafanya kazi yake. Yeye anajaribu kuiba furaha yetu, amani yetu, na umoja wetu. Yeye anataka tutenganishwe kutoka kwa watu wa Mungu, tutenganishwe na wale ambao wanaweza kutusaidia ili tupate nguvu zaidi, na tutenganishwe kutoka kwa wale ambao wanaweza kutuunga mkono.

Adui yetu anafanya vita dhidi yetu kutoka pande mbali-mbali maishani, na yeye anawavamia watu wa Mungu kwa vishindo. Yeye kwa kweli hana heshima na mtu yeyote. Kama wewe unaishi kwa ajili ya Mungu lengo la adui yetu ni kukufanya kuwa mwathiriwa wake—maanake uwe majeruhi katika vita hivi vya kiroho. Adui yetu anafanya vita dhidi ya watu katika maisha yao ya kibinafsi; anavamia ndoa zao, familia zao, na hata makusanyiko ya kanisa. Basi hebu tufungue macho ili tumtambue adui yetu wa kweli. Sasa si wakati wa kuingiwa na hofu na kujikunyata kutokana na mavamizi yake. Badala yake tunahitaji kumpinga huku tukisimama wima katika imani!

Yesu aliwaambia wanafunzi wake “Kesheni,
(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)



“Shetani... anajaribu kufanya Wakristo kuishi kwa woga na kufanya juu chini kuua, kuiba, na hata kuangamiza maisha yetu ya kiroho.”

Ibilisi, Kama Simba
Angurumaye

1

Tahariri

3

Mafundisho ya Biblia:
Usalama wa Milele

4

Usalama wa Milele
5-6

Swali na Jibu:
Marejesho

7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

8

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa

1)

mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho iko radhi, lakini mwili ni dhaifu” (Mathayo 26:41). Sisi tungali katika mwili na hatuna budi kuyapata majaribu wakati tungali tunaishi ulimwenguni. Kwa kweli bado hatujafika mbinguni ndiposa tunahitaji kukesha na kuomba ili tusikose njia ya wokovu na kurudi ulimwenguni. Maombi ndiyo silana ambayo itatuwezesha kushinda mavamizi ya adui yetu. Nayo miili yetu ni dhaifu sana na shauku letu kwa Mungu halitoshi kutulinda kutokana na nguvu za adui yetu. Basi tunahitaji kuwa macho na kuendelea kutafuta neema na nguvu kutoka kwake Bwana bila kukoma.



“Shetani amewataka ninyi
apate kuwapepeteta kama vile
ngano; lakini nimekuombea
wewe ili imani yako isipungue.”

Yesu alimwambia Petro katika Luka 22:31-31 “Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeteta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isipungue; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako.” Hata sasa Shetani angali ana shauku ya kukupata WEWE! Lakini Yesu anakwombea na kufanya sala kwa ajili yako akiwa katika mkono wa kuume wa Mungu. Nazo habari njema ni kwamba nguvu zake Mungu ni kuu zaidi kuliko nguvu za Ibilisi. “Aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia” (1 Yohana 4:4). Kama wewe utasimama wima pamoja na Mungu kila siku Yeye atakulinda na kukupatia

usalama na kukupatia njia ya kushinda nguvu za Ibilisi, lakini unahitaji kuwa macho na pia kuwa mwangalifu katika mambo ambayo utachagua kufanya, na pia kwa maamuzi utakayofanya maishani. Mwanga wa Neno la Mungu utadhihirisha mipango ya adui yetu, naye Mungu atafanya njia ya sisi kuweza kuepuka kila jaribu na kufanya njia katika kila bonde na kila mlima ambao utaletwa na adui yetu.

Hata ingawa tunahitaji kuwa waangalifu hatuna haja ya kuishi kwa kumwogopa adui yetu wakati ambapo nguvu zake Kristo zipo juu yetu. “Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru” (Luka 10:17-19). Wewe una uwezo (na kwa kweli utaweza) kuyashinda mavamizi ya adui yetu mradi ukiendelea kudumisha imani yako na kuamini nguvu zake Yesu Kristo. Wakati vita hivi vinaendelea, na wakati tukiendelea kumpinga ibilisi huku tukisimama wima katika imani yetu, kuna usalama mkubwa katika neema ya kutuokoa, ambayo inapatikana ndani yake Yesu Kristo. Neema hiyo yatoshwa kutufikisha huko Mbinguni ambako ndiko nyumbani kwetu tukiwa salama salimini. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the-gospeltruth.org

Tahariri



Basi, limesalia pumziko la sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika pumziko lake amepumzika mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyopumzika katika kazi zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika pumziko lile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.—Waebrania 4:9-11

Somo letu katika robo hii ya mwaka linashughulikia swala la kithiolojia la usalama wa milele, swala ambalo linasema kwamba “ukiokoka, umeokoka milele.” Mafundisho haya kuhusu usalama wa milele ni moja ya kanuni za kimsingi za mafundisho ya Ukalvini (Calvinism). Nayo mafundisho ambayo yalikuwa kinyume na hayo ya Ukalvini ni yale ya Uaminiani (Arminianism). Kambi hizi mbili tofauti za kithiolojia zimegawanyika kuhusiana na maswala ya utawala wa Mungu, upotevu wa mwanadamu, uchaguzi wa Mungu, utakaso wa Kristo, neema, uwezo wa mwanadamu wa kufanya uchaguzi, na pia swala la kuwa na uvumilivu maishani. Maswala haya yote yameshikamana, kwa maana utapata moja ya swala hizo linaguzia yale mengine. Lakini kwa sababu gazeti hili ni ndogo mimi sitaweza kushughulikia maana tofauti tofauti ambazo zimetolewa katika maandiko ambayo yanashughulikia maswala haya, badala yake nimelazimika kushughulikia maandiko hayo kwa njia ya moja kwa moja kwa njia ya kimuhstasari. Hata ingawa mimi ninaamini kwamba mafundisho ya Uaminiani ndiyo ambayo ni ya kweli zaidi kuliko Ukalvini, mwongozo mkubwa na unaofaa zaidi ni ule unalingana na Maandiko yenyewe, na hatuna haja ya kuongozwa na mafundisho fulani ya kithiolojia ambayo yametokana na ushawishi wa aina moja au nyingine. Kusema kweli kuna ukweli mdogo mdogo ambao unaweza kupatikana katika mafundisho hayo yote mawili na mwanathiolojia anayejaribu kutafuta tofauti (zote) zilizoko katika itikadi hizi zote mbili za Ukalvini na Uaminiani anaweza kupoteza njia.



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na


kupata jarida

za mbele.

Fundisho linalosema kwamba “Ukiokoka, umeokoka milele” ni dhana ambayo kwa kweli haitokani na Mungu, na pia ni ambayo inaweza kufanya watu kujihisi usalama ambao sio wa kweli. Hili ni fundisho ambalo linafungua mlango wa watu kukubali dhambi maishani mwao huku wakitumia neema kama mwavuli wa kujifunika. Hata ingawa mafundisho haya hayalingani na Biblia kunayo maandiko mengi ya kimsingi ambayo yanatumiwa na Wanakalvini ambayo ni ya msaada mkubwa wa kumsaidia mtu kuelewa mpango wa Mungu wa wokovu kwa njia inayofaa. Mungu amewaita watoto wake kuingia katika maisha ya utakatifu huku wakijitenga na dhambi za kitabia ambazo humtenganisha mwanadamu na Mungu. Kungali kuna nafasi kubwa ya mtu kukua ndani yake Bwana na katika kutimiza utakatifu wote. Kama hatutakuwa waangalifu Kanisa la Mungu linaweza kutilia mkazo zaidi swala la matendo mema hivi kwamba watu wataanza kujitambua na kujisikia salama kutokana na matendo yao ya kibinafsi kama Wakristo. Lakini hata ingawa matendo mema yanatokana na wokovu wa kweli, matendo mema yenyewe hayawezi kumwoko mwanadamu, na kamwe hayawezi kudumisha wokovu wetu. Sisi huokolewa kutokana na neema ya Mungu na kupitia kwa utakaso wa damu yake Yesu. Kuna usalama mkubwa zaidi unaotokana na mtu kutambua kwamba Mungu yuko tayari kutusamehe dhambi zetu na kuturudisha katika njia ya haki badala ya kututupa nje yake. Kwa kweli mtu kujihisi kwamba ana utakatifu wa kibinafsi ni jambo ambalo huwa ni matokeo ya mtu huyo kutilia mkazo matendo mema kama chanzo cha utakatifu wake.

Wokovu ni kazi ya Mungu ambayo hutuweka huru kutokana na nguvu za dhambi. Waalimu wa usalama wa milele mara nyingi hutilia mkazo ukweli kwamba wale ambao hawaamini usalama wa milele huwa wanaweka udhaifu nguvu za damu ya Yesu na neema yake Mungu. Lakini mimi ninaamini kwamba kuna ukweli mkuu zaidi ambao mtu anaweza kupata kwa kutumia maandiko hayo hayo. Je, si itakuwa ni kupatia damu ya Yesu na neema yake Mungu uwezo zaidi ikiwa tutaamini kwamba kupitia kwake sisi hatutarudi dhambini? Kazi yetu ni kudumisha imani kwa nguvu zake Mungu ambazo zinaweza kutudumisha, na pia kutii neno lake kupitia kwa neema yake, ambayo ndiyo inatuwezesha kutimiza hayo yote.

Neno la Mungu limesema waziwazi kwamba watu wanaweza kuteleza na kutoka katika imani na kupoteza uzima wa milele ikiwa wao hawatadumisha ushirika wao na Mungu. Ndiposa basi tunasema kwamba mafundisho kuhusu usalama wa milele sio ya kweli; lakini hata hivyo sisi hatutaki kufundisha fundisho lingine la uwongo la kusema kwamba kamwe hatuna usalama wa milele. Urembo wa wokovu ulio wa kweli ni kwamba kuna pumziko ambalo ni la watu wa Mungu wakati (wao) wameachana na kazi zao za kibinafsi. Mimi ninamshukuru Mungu kwamba nina usalama wa milele katika upendo na neema yake Mungu. Basi wewe hebu fanya huduma yako huku ukiendelea kuwa mwaminifu, na uchague usalama ambao ni mkuu zaidi ya mambo mengine yote ulimwenguni huu.



Michael W. Smith
Aprili 2019

Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: Usalama wa Milele

Somo la Biblia: *Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.*—Waebrania 10:38-39

Maana: Usalama wa milele, ambao kwa jina lingine kwenye thiolojia ya Kalvini unajulikana kama “kudumishwa kwa watakatifu,” —ama kwa maneno yanayojulikana sana unajulikana kama: “*ukiokoka, umeokoka milele,*” ni jambo ambalo limetafsiriwa kwa njia tofauti tofauti. Lakini kwa undani wake mafundisho haya yanasema kwamba kama kwa kweli mtu amehuishwa na kuzaliwa mara ya pili basi hakuna jambo lolote ambalo linaweza kubadilisha wokovu huo. Basi itikadi hii inasema kwamba kama mtu amempokea Kristo na kuokoka, basi Kristo atadumisha mtu huyo katika wokovu wake na kamwe wokovu huo hauwezi kumponyoka na hawezi kamwe kuupoteza.

Muhstasari: Wokovu wa mwanadamu unatokana na neema yake Mungu (peke yake) na kamwe hautokani na matendo ya mtu. Mungu atakuwa mwaminifu kumdumisha Mkristo katika neema yake ambayo humwezesha kuishi maisha matakatifu. Wokovu ni uhusiano wa imani ambao umetokana na agano; basi ikiwa mtu ataamua kutoka kwenye imani hiyo na akaacha kujitua kwa Mungu basi uhusiano huo utakuwa umekatika na wokovu humponyoka mtu huyo. Basi hata ingawa usalama wa milele au “*ukiokoka, umeokoka milele*” ni thiolojia ya upuzi, muumini anaweza kupumzika katika neema yake Mungu na kuwa na usalama wa milele ikiwa yeye ataendelea kumfuata Kristo kwa njia ya imani.

I. Wokovu Unatokana na Neema Kupitia kwa Imani

- A. Waefeso 2:8-9 Mmeokolewa kwa neema (Warumi 5:1).
- B. Warumi 7:25 Mungu huokoa kabisa.
- C. 2 Wakorintho 5:17 Viumbe vipya katika Kristo.

II. Uzima wa Milele ni Kipawa cha Mungu

- A. Yohana 5:24 Aminiye anao uzima wa milele (1 Yohana 5:11-13).
- B. Yohana 6:37-40 Ajaye kwa Yesu kamwe hatatupwa nje.
- C. Warumi 6:20-23 Mshahara wa dhambi na karama ya Mungu.

III. Usalama Ndani ya Mungu

- A. Yohana 10:27-29 Kondoo wa Kristo kamwe hawatapotea.
- B. Warumi 8:35-39 Hakuna kitakachotutenganisha na upendo wa Mungu.

IV. Mungu ni Mwaminifu Kudumisha

- A. Yuda 1:24 Yeye aweza kutulinda ili tusijikwae (1 Petro 1:5).
- B. 2 Wakorintho 1:22 Mungu hutia watu wake muhuri (Waefeso 4:30).
- C. 1 Wakorintho 1:8-9 Kuthibitishwa hadi mwisho.
- D. Wafilipi 1:6 Mungu atakamilisha kazi yake.

V. Maisha ya Kiroho Yakitolewa Mfano

Yohana 15:1-11 Mkristo anahitaji kudumu , ndani yake Kristo, ambaye ndiye Mzabibu wa Kweli.

VI. Utakatifu Ni Lazima

- A. 1 Wakorintho 6:9-11 Waovu hawataridhi ufalme wa Mungu.
- B. Waebrania 12:14-15 Fuateni utakatifu ndiposa msiingie unajisi.

- C. 1 Yohana 1:6 Kusema kwamba tunao ushirika na Mungu huku tukiwa tungali gizani basi twasema uwongo.

VII. Ushahidi Unaoonyesha kwamba Mtu Anaweza Kupoteza Wokovu Wake

- A. Mathayo 13:3-9 Mfano wa mpanzi.
 - B. 1 Timotheo 4:1 Wengine watajitenga na imani (Matendo 20:28-30).
 - C. Wagalatia 5:1, 4 Kuanguka kutoka kwa neema.
 - D. 1 Timotheo 6:9-11 Kufarakana na imani.
 - E. Waebrania 13:12-14 Kutokuamini humfanya mtu kujitenga na Mungu.
 - F. 1 Yohana 1:8-9 Msipoteze kile ambacho tayari mshatenda.
 - G. Ufuno 3:3-6 Mavazi machafu.
 - H. 2 Petro 2:20-22 Kunaswa na Kushindwa.
 - I. 1 Wakorintho 3:16-17 Mungu ataangamiza hekalu ambalo limeharibika.
- Tazama pia:** 1 Wakorintho 9:27; 2 Petro 3:17; Warumi 11:21-23; 2 Timotheo 2:17-19.

VIII. Wito wa Kuwa Waaminifu

- A. Wakolosai 1:21-23 Msigeuzwe na kuacha imani.
- B. 1 Wakorintho 15:58 Mwimariki na msitikisike.
- C. Waebrania 4:14 Tuyashike sana maungamo yetu (Waebrania 3:14).
- D. 1 Timotheo 6:12 Shika uzima wa milele.

Tamati

Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.
—Ufunuo 2:10b

UONGO ULIOKO KATIKA MAFUNDISHO YA USALAMA WA MILELE



Kuna mgawanyiko mkubwa ulioko kati ya Wakristo kuhusu mafundisho ya usalama wa milele. Je, inawezekana mtu akishampokea Kristo akapoteza tena wokovu wake ama wokovu ni jambo la hakika hata kama mtu huyo atarudi dhambini?

Mpango wa Wokovu

Maswali kuhusu usalama wa milele ni mengi na majibu ya maswali hayo yanaguzia maswala mengine mengi ya kithiolojia. Hata ingawa kuna mgawanyiko mkubwa kati ya wanathiolojia na hata ingawa kuna maandiko ambayo yanatumia kuunga mkono mielekeo ambayo ni tofauti kabisa, maandiko yenyewe kwa ujumla hayafundishi itikadi ambazo ni tofauti. Kwa wingi Biblia inatuhadithia mpango mzuri wa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu ambao unatokana na angano na pia hutokana na imani. Kwa kweli msimamo wake Mungu ni ule ambao unalingana na Neno lake, na Yeye atakuwa ni mwaminifu kwa watoto wake. Lakini ili uhusiano

“Waumini wanaweza kuwa na uhakika kwamba neema ya Mungu ambayo ndiyo inaturudishia uhusiano ambao mbeleni ulikuwa umevunjika inatosha kutudumisha katika uhusiano huo.”

huo uwe mkamilifu inabidi watoto wake waendeleo katika uchaguzi wao wa kumfuata Kristo bila kuhesabu gharama yake. Muumini anayeokoka huendelea kuwa na uwezo wa kufanya uamuzi wa kutoka kwenye imani yake na kurudi katika maisha ya dhambi. Lakini kwa kufanya uamuzi huo wa kibinafsi muumini huwa ameachana na wokovu na kupoteza faida za wokovu huo.

Mafundisho ya Uongo Yanatoa Idhini kwa Mtu Kuendelea Kutenda Dhambi

Wakati mwingi mafundisho kuhusu usalama wa milele yanajulikana kama: “ukiokoka, umeokoka milele.” Lakini mafundisho haya

hufungua mlango wa watu kuendelea kutenda dhambi huku wakijidai kwamba wameokoka, na pia yanawatumbukiza watu katika mchanganyiko wa kithiolojia wa kudai kwamba kama mtu atarudi dhambini basi hakuwa ameokoka tangu mwanzo. Lakini misimamo yote hii miwili hailingani na Neno la Mungu. Hata ingawa mafundisho ya usalama wa milele si ya kweli, kuna kweli muhimu ambazo zinapatikana katika mafundisho hayo. Basi tunahitaji kuwa waangalifu ili tusimwage nje kweli muhimu, eti kwa sababu mtu fulani

ametumia nguzo za Neno la Mungu kujenga mjengo usiofaa.

Wokovu ni kwa Neema, Sio kwa Kazi za Mtu

“Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu” (Waefeso 2:8-9). Wokovu hautokani na matendo ya mtu bali ni kazi ya Mungu peke yake, na pia ni kipawa cha neema yake Mungu, wakati mtu ameweka imani na tumaini lake katika Bwana Yesu Kristo. Wokovu wa Yesu ni kamili na Yeye huokoa kabisa (Waebrania 7:25). Kuna pumziko kubwa ambalo mtu hupata kwa kutambua kwamba wokovu haupatikani kutokana na wema wa kibinafsi bali unatokana na neema kubwa ya rehema za Mungu. Mafundisho ambayo hutumiwa sana kufundisha kuhusu usalama wa milele huwa hayafai kufanya hivyo; lakini hata ingawa matendo mema huwa ni tunda la imani ya kweli, wokovu unapatikana kutokana na neema, na sio kutokana na mtu kustahili. Inambidi Mkristo kuendelea kujitolea kwa utakaso wa Kristo ambao ndio pekee unafaa. Waumini wanaweza kuwa na uhakika kwamba neema ya Mungu ambayo ndiyo inaturudishia uhusiano ambao mbeleni ulikuwa umevunjika inatosha kutudumisha katika uhusiano huo.

Matokeo ya Uwezo wa Kufanya Uchaguzi

Yohana 6:37-40 inasema kwamba yeyote yule ambayo anakuja kwa Yesu hatatupwa nje na waaminio watakuwa na uzima wa milele. Andiko hili halisema kwamba mtu hawezi kupoteza imani yake bali linanena kuhusu karama ya uzima wa milele ambayo inatolewa kwa wale ambao wanamwamini Bwana Yesu. Baadaye katika sura hiyo tunasoma kwamba wengi wa wanafunzi wa Kristo walirudi nyuma wasitembee naye tena. Wanadamu daima huwa na uwezo wa kuamua kumtoroka Mungu, na kwa tendo hilo kuacha wokovu wao. Nayo Yohana 10:27-29 inakili Yesu akiwapa kondoo wake uzima wa milele na kwamba “hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu.” Hakuna mwanadamu au nguvu zozote zile zenye uwezo wa kututoa kutoka mkononi mwake bali sisi wenyewe ndio tunaweza kuiba kipawa cha wokovu ambao Mungu ametukabidhi; kwa maana

(Endelea katika Ukurasa 2)

(Inaendelea kutoka Ukurasa

5)

kondoo ambao alinena kuwahu ni wale ambao husikia sauti yake na kumfuata (aya ya 27). Lakini ikiwa kondoo hao watakoma kumfuata kwa hiari yao wenyewe, basi kwa uamuzi wao watakuwa wameondoka kutoka kwa usalama wa mikono yake Baba.

Kuna pumziko kubwa linalotokana na ufahamu kwamba hakuna chochote kile ambacho chaweza kututenganisha na upendo wake Mungu (Yohana 8:35-39). Uchaguzi wetu ndio jambo la pekee ambalo huvunja uhusiano wa imani na upendo wakati Roho wa Mungu amerudisha uhusiano huo mahali pake. Matokeo ya uchaguzi huo kwa kila mmoja wetu ni: “Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu” (Warumi 6:23).

Mungu Anaweza Kutudumisha Ili Tusianguke

Maandiko mengi hunena kuhusu uaminifu wa Mungu na uwezo wake wa “kutulinda ili tusijikwae.” Mungu huweka watu wake muhuri (2 Wakorintho 1:22) na kuwadumisha na hata kuwapa usalama dhidi ya uovu wa ulimwengu, mradi tu wao wanadumisha imani yao kwa njia ya kumfuata Kristo. Yesu alitoa mfano wa uhusiano huo kwa njia ya mfano wa mzabibu na matawi yake, mfano ambao hupatikana katika Yohana 15:1-11. Ikiwa tawi halizai matunda mema basi

tawi hilo hukatwa na kutupwa nje. Sisi tumepewa amri kwamba “tudumu” katika Kristo. Kama hatutadumu ndani yake Kristo basi tutatupwa nje na kuchomwa. Matunda yote ya wokovu na utakatifu wote hutokana na mtu kudumu ndani yake Kristo, kwa maana bila yeye hatuwezi kufanya jambo lolote. Kama muumini ataacha kudumu ndani yake Kristo uhusiano huo hukatika na matokeo yake ni maangamizi ya milele badala ya uzima wa milele.

Biblia inasema dhahiri kwamba waovu hawataridhi ufalme wa Mungu (1 Wakorintho 6:9-11). Kama mtu amekiri imani yake kwa Kristo na kuokoka na baadaye akarudi kwenye matendo ya kimwili basi yeye huwa amepotea kiroho. Waebrania 12:14 nayo inafundisha kwamba hatutaweza kumwona Mungu bila kuwa watakatifu. Utakatifu wa kweli hutoka kwa Yesu lakini ikiwa tutamwacha Yesu basi hatutakuwa watakatifu, na ikiwa hatutakuwa watakatifu hatutaweza kumwona Baba. Mstari wa 15 unasema, “Mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo.” Basi ni dhahiri kwamba Mkristo anahitaji kuendelea

kukubali kazi ya neema ya Mungu maishani mwake, asipofanya hivyo basi matokeo yake yatakuwa kukosa njia na yeye kuingia unajisi. Kusema kweli ukweli huo uko kinyume na mafundisho ya usalama wa milele.

Onyo Dhidi ya Kurudi Nyumba


Kuna maandiko mengi katika Agano Jipya ambayo yanatuonya dhidi ya kuacha njia ya utakatifu na ambayo pia yanatoa ushahidi kwamba inawezekana mtu kupoteza wokovu wake na imani yake. Mfano wa mpanzi ambao unapatikana kaitika Mathayo 13:3-9, unadhihirisha ukweli kwamba watu wanaweza kuokoka kwa muda lakini majaribu yajapo mbegu iliyo ndani yao inafifia kwa maana hawakuruhusu neno la Mungu kupata mizizi ndani yao. 1 Timotheo 4:1 inatukanya kwamba kuna wengine ambao “watajitenga na imani,” na pia Wagalatia 5:1 inatukanya kwamba tunahitaji kutahadhari kwa maana kuna hatari ya kunaswa “tena chini ya kongwa la utumwa.” Wayahudi ambao walirudi kutumikia sheria baada ya kupokea wokovu walikuwa “tayari wameanguka kutoka kwa neema” (mstari wa 4).

1 Timotheo 6:9-11 inasema kuhusu wale ambao “wamefarakana na imani.” Na katika Waebrania 3:12-14 watakatifu wanakanywa kuwa macho ili wasiondoke kutoka kwa Mungu kutokana na moyo mwovu wa kutokuwa na imani. Ikiwa muumini ambaye ni hekalu la Roho Mtakatifu atanajisi hekalu hilo ambalo wakati mmoja lilikuwa safi basi Mungu ataangamiza hekalu hilo (1 Wakorintho 3:16-17). Mungu alipatia makusanyiko ya Kitabu cha Ufunuo mweke wa kutubu kwa maana wengi wao walikuwa wameanguka na mavazi yao kuingia najisi. Nayo 2 Petro 2:20-22 inasema wazi wazi kuhusu wale ambao walikuwa wameokoka lakini wakanaswa tena na inaonyesha jinsi mwisho wao wa milele utakuwa mbaya zaidi kwa maana wamegeuka na kuacha ukweli.

Msitolewe Kutoka kwa Imani

Kuna ushahidi mwingi wa maandiko ambao unaonyesha kwamba hata baada ya watu kuokoka kungali kuna uwezo wa wao kuacha ile imani yao ya kwanza katika Kristo na kuondoka kutoka kwenye ujuzi wao wa wokovu. Ndiposa mara nyingi mitume waliwahimiza watakatifu na kuwaambia “Msigeuzwe na kuacha imani” (Wakolosai 1:21-23), “Mwimarike na msitikisike” (1 Wakorintho 15:58), na pia kwamba washike “uzima wa milele” (1 Timotheo 6:12).

Mafundisho kuhusu usalama wa milele yako kinyume na ukweli wa Neno la Mungu. Nguvu za Mungu zinatoshia kutudumisha ili tusitende dhambi na inatuwezesha kuishi maisha matakatifu kwa neema yake. Basi tunahitaji kuwa macho huku tukitegemea wema wa damu yake Kristo badala ya kutegemea wema wetu wa kibinafsi, na kumtumikia Mungu kwa utakatifu. Yeye anaweza kutudumisha kutokana na uovu wote wakati tukiruhusu utakatifu wake kufanya kazi katika kila sehemu ya maisha yetu. ■



“Kama muumini ataacha kudumu ndani yake Kristo uhusiano huo hukatika na matokeo yake ni maangamizi ya milele badala ya uzima wa milele.”

Swali na Jibu

Je, kulingana na Waebrania 6:4-6 na Waebrania 10:26-29 ni jambo lisilowezezana mtu ambaye alikuwa ameokoka hapo mbeleni halafu akaacha imani yake na kurudi dhambini kurudishwa wokovuni?

LA hash! Kwa kweli si jambo ambalo haliwezekani kwa muumini ambaye amerudi nyuma kurudia tena wokovu wake. Jambo la kimsingi katika injili ni ujumbe wa upendo mkuu wa Mungu kwa mwanadamu na tumaini la kurudishiwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu kupitia kwa damu yake Kristo. Petro wa Pili 3:9 inatwambia kwamba Mungu “hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.” Bwana hapendelei kwamba mtu yeyote kupoteza nafsi yake (milele); ndiposa Yeye hufanya juu chini kuhakikisha jambo hilo kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu ambazo ndizo humhakikishia mtu dhambi na kuvuta watu wote kuja kwake. Wito ambao umetolewa katika Ufunuo 22:17 ni kwamba, “Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure,” na mwito huo umetolewa hadi kwa Mkristo ambaye amerudi nyuma. Mara nyingi Agano la Kale limedhihirisha sifa zake Mungu za kutoa msamaha na kuonyesha jinsi Yeye alivyokuwa tayari kurudisha taifa la Israeli ambalo lilikuwa limeanguka na kulirudisha katika uhusiano bora naye. Hata ingawa kuna neema ya mtu kuishi kama Mkristo (mshindi) maishani, iwapo mtu atapoteza wokovu wake kutokana na dhambi yeye hatakuwa amepoteza tumaini kabisa mradi awe tayari kutubu na kumtii Bwana Yesu. Kusema kweli mwaliko wa kurudishiwa uhusiano na Mungu umetolewa kwa watu wote.

Hebu tuchambue maana ya Waebrania 6:4-6 na 10:26-29 kulingana na ukweli ambao umetajwa hapo juu. Maandiko haya mawili ya Waebrania yanafanana kwa maana na tafsiri. Waebrania 6:4-6 inasema: “Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.” Kijuuuu maandiko hayo yanaweza kuonekana kama kwamba yanasema wokovu hauwezekani tena kwa

watu ambao wakati mmoja walipata ujuzi wa nguvu za Mungu ambazo zilileta neema ya wokovu maishani mwao. Lakini mtu akisoma maandiko hayo kwa undani zaidi atapata ukweli tofauti. Tambua kwamba sababu iliyotolewa kwa ajili ya kusema kwamba “haiwezekani kuwafanya wanya wakatubu” ni kwa sababu hata sasa wao wanamsulubisha Yesu tena. Je, itawezekanaje watu kuokoka ikiwa wanaendelea kukana nguvu za damu yake Yesu? Ikiwa mtu amekana nguvu za Yesu ambazo humtoa dhambini basi haiwezekani yeye kufanywa upya mpaka hapo atakapofanya toba. Kama mtu ataacha kumsulubisha Kristo mara nyingine maishani mwake na kukubali nguvu za damu yake basi kuna nafasi ya yeye kurudishiwa uhusiano wake na Bwana, na asiwe tena wa kuleta aibu kwa Kristo. Lakini maandiko hapa hayaneni kuhusu waliorudi nyuma, bali yanazungumzia watu ambao wamekana na kukataa kabisa dhambi yake Kristo ambayo huleta utakaso.



Vile vile Waebrania 10:26 inasema kwamba: “Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhambi kwa ajili ya dhambi.” Andiko hili likisimama peke yake ni kama linaonyesha kwamba hakuna dhambi ya dhambi kwa yule mtu anayerudi nyuma, lakini maandiko yanayofuata andiko hilo yanadhihirisha maana ya mstari wa 26: “Bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?” (Waebrania 10:27-29). Maandiko hayo yanaweka wazi zaidi somo ambalo linapatikana hapa.

Hamna dhambi ya dhambi isipokuwa damu yake Yesu. Kama dhambi hiyo itachukuliwa kuwa sio takatifu na ambayo haiwezi kuleta wokovu basi hamna utakaso mwingine au dhambi nyingine ya dhambi ambayo inaweza patikana. Kutakuwa na adhabu kali kwa wale ambao walio-okoka halafu wakakataa damu ya agano. Basi maandiko yaliyopo hapa hayafundishi kwamba mwenye kurudi nyuma hawezi kurudishwa wokovuni, lakini yanafundisha kwamba wokovu hauwezi patikana ikiwa mwenye kurudi nyuma ataendelea kuikataa damu yake Yesu kama njia ya wokovu. “Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo” (Matendo 4:12). Wakati mtu aliyeikataa injili na kurudi nyuma atakapobadilisha moyo na kauli lake na kuikubali dhambi yake, Mungu atamwokoa kwa rehema na neema zake. ■



JE, WAJUA?

Asilimia 77% ya Wamarekani wote wanaamini kwamba mtu hupata wokovu wa kibinafsi kutokana na matendo mema.

Asilimia 52% wanasema kwamba matendo mema humsaidia mtu kuhifadhi mahali pake mbinguni.

Asilimia 60% wanaamini kwamba kifo cha Yesu Kristo msalabani ni dhabihu ya pekee ambayo yaweza kuondoa adhabu ya dhambi.

Habari hii imenakiliwa kutoka kwa utafiti unaojulikana kama: *The State of American Theology, LifeWay Research, 2016.*

Asilimia 65% ya “Wakristo” wote wanaamini kwamba kuna njia tofauti tofauti za mtu kufika Mbinguni.

Habari hii imenakiliwa kutoka kwa utafiti ujulikanao kama: *The State of American Theology, LifeWay Research, 2016.*



MKE WA MCHUNGAJI

Tazama, mjakazi wako ni mtumwa wa kuwaosha miguu watumishi wa bwana wangu.

—1 Samueli 25:41b

Majibu hayo ya Abigaeli wakati alipozwa na Daudi kwa ajili ya ndoa yanaonyesha jinsi Abigaeli alikuwa tayari kufanya huduma ya kiwango cha hali ya chini, hata kuwa tayari kufanya utumishi wa kuosha watu miguu. Kuna wake wengi wa wachungaji ambao kila siku huishi kulingana na maneno hayo ya Abigaeli. Wao hufanya kazi bila malipo na hata bila kufanya makelele ya kutaka kutambuliwa, huku wakitumikia watu ambao wamewazunguka. Maisha ya mke wa mchungaji yana changamoto za aina spesheli sana na ndiposa yeye anahitaji kupewa heshima na kutukuzwa kutokana na maisha yake ya huduma na ya kujitolea hapo kanisani. Wake wa wachungaji huwa na wajibu muhimu katika mwili wa Kristo na wao wanastahili kupewa heshima kuu.

Mke (wa kawaida) wa mchungaji “anatarajiwa” kuwa amepanga kila kitu kanisani kikawa laini, aonekane wa kupendeza, akae pale mbele wakati wa ibada, awe mchangamfu na mwenye tabasamu usoni, awe mke kamili, awe na watoto ambao kamwe hawatakuwa na tabia mbaya na ambao ni Wakristo wa kuigwa, awe tayari kubadilisha mipango yake bila kunzunguka kwa manufaa ya kanisa, na awe na ushuhuda ambao hauonyeshi kwamba ana changamoto ya kuishi kama Mkristo, na hata kukosa kudhihilisha uwanadamu mwingi maishani mwake. Jameni! Matarajio haya yote ni changamoto lenye kuleta masumbufu mengi katika maisha ya mke wa mchungaji, ambaye tayari kazi yake kila wakati huwa ni nyingi na juu ya hayo yeye ni mama mzazi.

Wake za wachungaji ni wanadamu na wana mahitaji kama kila mtu mwingine kanisani. Wao hujihisi kuwa na upweke na pia kujihisi kwamba hawana nguvu za kufanya huduma wanayotarajiwa kufanya. Wao pia hujihisi kwamba wanatazamwa na kila mtu na kwamba hata hawana maisha ya kibinafsi. Kila wakati wao huwa na msukumo wa kutimiza matarajio makuu ya washirika wa kanisa.

Mke wa mchungaji ambaye ni mwaminifu kwa wito wake ni mfanyi kazi mwenye bidii na ambaye majukumu yake ni zaidi ya kuwa mke na mama wa watoto wa mchungaji. Yeye huwapikia wagonjwa, anawafundisha watoto, anawaalika wageni nyumbani mwake, anaandaa mankuli ya Jumapili jioni kwa ajili ya wageni, huwapa wosia na kuwaombea wale ambao wana mahitaji, hujibu simu za wale wanaompigia, na pia kujibu wenye kumtumia ujumbe mfupi, husafisha na kurembesha kanisa, na anawakilisha mumewe katika majukumu mbali mbali, na kadhalika.

Moja ya kazi ngumu sana na yenye changamoto sana ambayo mke wa mchungaji hufanya ni ile ya kuwa rafiki, msiri, mwenye jukumu la kusikiliza mipango ambayo mchungaji yuko nayo. Yeye husikiliza masumbufu makali na changamoto zinazomkabili mumewe mchungaji. Yeye huona waziwazi maumivu ambayo watu humsababishia mchungaji. Yeye hutazama jinsi ambavyo mchungaji hujikaza kisabuni katika hudumu lakini anachopata kutoka kwa washirika ni lawama tupu. Yeye basi hufanya juu chini ili kupata msamaha wa Kristo ili aweze kuendelea kupenda na kuwatumikia wale ambao wanamdhuru mumewe kwa maneno yao.

Asilia 80% ya wake wa wachungaji husema kwamba wao hujiona kwamba washirika wa kanisa hawathamini kazi yao. Basi sasa mimi mwenyewe nasema kwa wake zote wa wachungaji: asanteni sana kwa yote ambayo mnafanya. Sisi hatuwatarajii nyinyi kuwa wakamilifu na tunatambua uwanadamu wenu kama tunavyotambua uwanadamu wetu wenyewe. Asanteni kwa kuendelea kutumika. Asanteni kwa kutupenda na kutuombea hata wakati ambapo matendo yetu kwenu sio ya upendo. Asanteni sana kwa kusimama na mume wako ambaye ni mchungaji wetu. Asante kwa ajili ya upendo wenu wa kiungu na hata huduma yenu. Sisi tunawapenda na kufurahia kazi yenu! ■